# Uratibu wa kibinadamu na mbinu za vikundi (cluster):

## mwongozo wa haraka kwa mashirika ya eneo na kitaifa

Mwongozo huu umeundwa kukusaidia kuelewa mbinu za kibinadamu kwa njia ya vikundi. Mwongozo huu hutoa muhtasari wa wenyewe ni nini na kwa nini shirika lako linapaswa kushiriki.

Global Education Cluster

TRANSLATORS WITHOUT BORDERS

Save the Children

Mwongozo huu ulitolewa na Translators without Borders (Watafsiri wasio na Mipaka) kwa kushirikiana na Gobal Education Cluster Localization Task Team (Timu ya Kazi ya Ujanibishaji ya Kikundi cha Elimu Duniani) na kwa ufadhili wa Shirika la Kuwaokoa Watoto (Save the Children). Unaweza kupata toleo linaloweza kuhaririwa la mwongozo huu kwenye tovuti ya Kikundi cha Elimu Duniani ambalo unaweza kurekebisha kulingana na muktadha wako.


# Mbinu ya vikundi ni nini?

Ni seti ya miundo, michakato, kanuni na ahadi za kuratibu hatua za kibinadamu wakati serikali ya kitaifa inaomba msaada wa kimataifa. Huwa unalenga kuifanya jamii ya kibinadamu kupangwa vizuri na kuwajibika zaidi kwa watu walioathiriwa na janga.

# Vikundi ni nini?

Vikundi ni makundi ya hiari ya mashirika ya kibinadamu yanayofanya kazi katika sekta maalum za kiufundi za hatua za kibinadamu, zilizoonyeshwa kwenye sehemu ya bluu iliyokolea kwenye mchoro hapa. Washiriki wa vikundi wanaweza kujumuisha mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya Umoja wa Mataifa, Msalaba Mwekundu /Harakati za Red Crescent, na taasisi za serikali zinazohusika katika kukabiliana na hali za kibinadamu. Wao huratibu hatua ili kuhakikisha matokeo bora kwa watu walioathiriwa na janga, katika hatua zote zilizoonyeshwa kwenye mishale katika mchoro. Vikundi huendeleza mkakati wa kawaida na mazoea mazuri, huepusha marudio, hushughulikia mapungufu na hushiriki taarifa. Huwa vinaunda uwezo wa kitaifa ili kujiandaa kwa hali za dharura, na kutetea hatua ya kibinadamu na yenye uwajibikaji. Vikundi vyote vinawajibika kusimamia kanuni za ulinzi na kuzuia unyanyasaji wa kijinsia, kutumiwa vibaya na kudhulumiwa.

Kuna vikundi 11 duniani. Vikundi vilevile vinaweza kuamilishwa katika kiwango cha kitaifa na wakati mwingine katika kiwango cha chini katika kitaifa ili kukabiliana na hali fulani ya dharura. Kila kikundi cha kimataifa kinaongozwa na shirika moja au mashirika mawili ya Umoja wa Mataifa au shirika la Umoja wa Mataifa na Shirika Lisilo la Kiserikali la kimataifa. Katika kiwango cha nchi, vikundi kawaida huongozwa pamoja na shirika la Umoja wa Mataifa na Shirika Lisilo la Kiserikali (NGO). Viongozi wa vikundi lazima wawe tayari kutoa huduma kwa watu walioathirika ambapo mashirika mengine hayawezi.




Kikundi cha Elimu kinaongozwa kwa pamoja na Fedha za Watoto za Umoja wa Mataifa (UNICEF) na Shirika la Kuokoa Watoto (Save the Children) katika kiwango cha kimataifa. Kikundi cha ushauri wa kimkakati pamoja na pembejeo za mashirika ya sehemu na ya kitaifa katika maswala ya kipaumbele. Katika kiwango cha nchi, vikundi vya elimu kawaida huongozwa na Mfuko wa Watoto wa Umoja wa Mataifa (UNICEF) na Shirika la Waokoe Watoto (Save the Children), lakini Shirika Lisilo la Kiserikali (NGO) lingine pia linaweza kuongoza.

# Kwa nini shirika langu linapaswa kujiunga na mfumo wa vikundi?

Ingawa una mapungufu kadhaa ya kiutendaji, mfumo wa vikundi unaweza kuwezesha shirika lako kuwahudumia vizuri watu walioathirika kupitia:

- Kuongezeka kwa ushawishi, kujulikana, na uelewa wa taratibu
- Fursa za ufadhili
- Upatikanaji wa mwongozo wa kiufundi na misaada
- Ufikiaji wa habari kuhusu kile wengine wanakifanya na mapungufu yoyote
- Fursa za ushirikiano na mashirika mengine

## Je, shirika langu linaweza kuwa na ushawishi mkubwa kwa kujiunga na kikundi?

Shirika moja pekee linaweza kupambana katika kushawishi sera za Umoja wa Mataifa, wafadhili na mamlaka ya kitaifa. Kwa mfano, unaweza kuhisi kuwa mipango ya ushirikiano ya Umoja wa Mataifa haieleweki, kwamba mahitaji ya wafadhili kwa mapendekezo ya ufadhili yana vizuizi sana, au kwamba mamlaka ya kitaifa yanazuia ufikiaji wa hali za kibinadamu bila sababu. Unaweza kuwashawishi kwa urahisi zaidi kwa kufanya kazi na mashirika mengine husika. Unaweza pia kuongeza mwonekano na athari ya shirika lako kwa kuchangia katika kazi ya pamoja ya kikundi, kujiunga na vikundi vyake vya kazi vya kiufundi au kikundi cha ushauri wa kimkakati, au kuongoza kikundi pamoja.

## Je, shirika langu linaweza kupata ufadhili kupitia kikundi?

Vikundi havitoi fedha moja kwa moja, lakini washiriki wa vikundi wanapata njia za ufadhili ambazo wasio wanachama hawawezi kupata. Kwa mfano, kwa ujumla unaweza tu kuomba msaada wa ruzuku ya pamoja uliokusanywa nchini ikiwa wewe ni mwanachama wa kikundi. Kuwasilisha mahitaji ya programu kwenye kikundi husika kunaweza kuonyesha mapungufu muhimu ya ufadhili kwa wafadhili. Wafadhili pia mara nyingi wanatarajia mashirika wanayoyafadhili kuonyesha kwamba miradi yao inaambatana na mikakati ya vikundi.

Vikundi husaidia kuamua jinsi ya kutenga pesa zilizojumuishwa nchini, ambazo zinachanganya michango ya kifedha ya wafadhili kadhaa. Shirika la uratibu wa misaada ya kibinadamu la Umoja wa Mataifa, Ofisi ya Uratibu wa Masuala ya kibinadamu (Office for Coordination of Humanitarian Assistance /OCHA), hutenga fedha hizi kwa miradi mingi katika kiwango cha nchi. Vikundi pia huunda malengo, shughuli na bajeti zinazoambatana kwa sekta zao maalum kama sehemu ya Mipango ya Kukabiliana na Hali za Kibinadamu. Wafadhili hurejelea haya ili kukuza vipaumbele vyao vya ufadhili.

## Je, shirika langu linaweza kupata msaada wa kiufundi kwa kujiunga na kikundi?

Waratibu wa kikundi na washiriki wa kikundi wanaweza kuwa na uwezo wa kutoa ushauri unaohusiana na maswala ya kiufundi ambayo ni mapya kwako. Mnaweza kufanya vivyo hivyo kwa washiriki wengine. Vikundi kadhaa pia vina ofisi za usaidizi za mtandaoni za kujibu maswali ya wanachama na wengine hutuma mtaalamu wa msaada wa kiufundi ambapo kikundi cha kitaifa hubainisha hitaji.

---

Ofisi ya Usaidizi ya Kikundi cha Elimu cha Kimataifa inaweza kujibu maswali na maombi mengine ya msaada kuhusu uratibu wa kiufundi na usimamizi wa taarifa. Hii ni pamoja na kushiriki rasilimali zinazofaa, zana na mwongozo, au kuelekeza ombi kwa mtaalam kwa usaidizi zaidi. Ofisi ya usaidizi inaweza kufikiwa kupitia barua pepe au Skype (help.edcluster). Ofisi hiyo ya usaidizi hupokea maombi katika lugha ya Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa na Kihispania.

---

Miongozo mingi ya kiufundi iliyo maalum na ya kisekta pia inapatikana mtandaoni na huhitaji kuwa mshiriki wa kikundi ili kuipakua. Kwa mfano, Kitabu cha Mwongozo (Sphere) kinajumuisha viwango vya chini vya hali za kibinadamu kwa maji, usafi wa mazingira na usafi wa mwili, usalama wa chakula na lishe, makao na makazi, na afya, na kinapatikana katika lugha zaidi ya 35.

---

Viwango vya chini vya Elimu vya INEE: Kujiandaa, Mwitikio, Ufufuaji hutoa msingi bora wa elimu ya kukabiliana na hali. Mwongozo zaidi wa kiufundi uliopendekezwa kwa mashirika yanayotekeleza mipango inayohusiana na elimu inaweza kupatikana kwenye tovuti ya INEE na katika maktaba ya Kikundi cha Elimu cha Kimataifa.

---

## Ninaweza kupata habari gani kutoka kwa kikundi?

Vikundi vinazalisha zana za usimamizi wa taarifa kama "4Ws", ambazo huonyesha Nani anafanya Nini, Lini na Wapi. Hivi vinaweza kusaidia shirika lako kufanya maamuzi bora kuhusu mipango gani ya kufanya na wapi. Vikundi pia vinawajibika kuandaa tathmini ya mahitaji na uchambuzi wa mapungufu kama msingi wa vipaumbele vya ufadhili na mikakati ya kukabiliana na hali. Unaposhiriki habari kulingana na ufahamu na utaalam wa shirika lako, unaweza kusaidia kupata suluhisho kwa maswala makubwa na kuboresha ubora wa jumla na uwajibikaji wa kukabiliana na hali.

## Je, ninaweza kupanua ushirikiano wangu kwa kujiunga na kikundi?

Unaweza kuunda uhusiano na mashirika yanayoongoza vikundi na washiriki wengine wa vikundi, pamoja na mamlaka ya kitaifa. Hii inaweza kukuruhusu kubadilishana taarifa na mashirika yenye nia za kufanana na utaalam wa ziada kama shirika lako mwenyewe. Uhusiano thabiti pia unaweza kusababisha ufadhili wa pamoja na ushirikiano wa utetezi, na mashirika ya kimataifa na ya kitaifa. Kanuni za Ushirikiano zinazokubalika sana zinaonyesha umuhimu wa usawa na uwazi katika mahusiano haya.

## Ni nini kinachohusika katika kuwa mshiriki wa kikundi?

Hakuna vigezo vya ushirika wa kudumu au michakato ya maombi ya kujiunga na kikundi, lakini kuna mambo ambayo unapaswa kuzingatia.

- Uwekezaji wa wakati kwa ushiriki endelevu: uwezo wa kuhudhuria mikutano ya mara kwa mara, pembejeo kwa ukuzaji wa mkakati, kushiriki habari zinazofaa na kwa wakati kwenye mikutano na zana kama 4Ws, toa utaalam wa kiufundi wakati unapohitajika, chukua uongozi wa pamoja pale inapofaa, onyesha vipaumbele vya utetezi
- Umuhimu wa kazi yako: utekelezaji wa programu unaofaa sekta moja au zaidi
- Masharti ya kiwango cha chini: shirika lako linapaswa
  - Kushikilia kanuni za kibinadamu za ubinadamu, kutounga mkono upande wowote, kutopendelea na uhuru
  - Kujitolea kwa mwongozo maalum wa kikundi na ulinzi wa kawaida katika programu zote, pamoja na kuheshimu kanuni za kutobagua na "usidhuru"
  - Kuwa tayari kushiriki katika vitendo ambavyo vinaboresha uwajibikaji kwa watu walioathiriwa, kulingana na Ahadi za Uwajibikaji kwa Kundi la Watu Walioathirika na Kanuni kuu Sita Zinazohusiana na Unyanyasaji wa kingono na Dhuluma.

---

Mikutano na hati za kikundi kwa kawaida huwa katika lugha kuu rasmi ya nchi au katika lugha za kimataifa kama Kiingereza na Kifaransa. Masharti ya kiwango cha chini ya uratibu wa vikundi yanasema kwamba vikundi vinapaswa kutoa ukalimani katika lugha inayofaa (ikijumuisha lugha ya ishara) ili washirika wote wa kikundi washiriki, ikijumuisha mashirika ya eneo. Kwa bahati mbaya hii sio zoezi la kawaida bado, lakini vikundi vingine katika hali tofauti vinafanya juhudi kuihusu.

---

## Je, shirika langu linaweza kujiunga na mfumo wa vikundi aje?

- Tafuta ni kikundi (cluster) au vikundi (clusters) vipi vinavyohusiana sana na kazi yako. Angalia humanitarianresponse.info au reliefweb.int kwa orodha ya vikundi vinavyofanya kazi na maeneo yao ya uwajibikaji. Wakati mwingine, unaweza kupata habari hii pia kwenye tovuti ya wakala wa serikali anayehusika katika nchi yako.
- Tafuta vipaumbele vya kimkakati kwa vikundi hivyo nchini mwako na uone ni vipi vinafaa zaidi kwa shughuli za programu yako: hii itakusaidia kutanguliza majadiliano unayoshiriki. Hati ya mkakati inapaswa kupatikana kwenye tovuti zilizo hapo juu. Hoja kuu za mkakati pia zitachapishwa kama sehemu ya Mpango wa Kukabiliana na Hali za Kibinadamu katika nchi yako, zinazopatikana pia kwenye tovuti hizo.
- Tambua mmoja au zaidi ya wafanyakazi wako waandamizi wenye maarifa husika ya kiufundi ili kufanya kazi nao kila wakati na vikundi hivyo.
- Tambua waratibu wa vikundi husika katika nchi yako kutoka kwenye tovuti zilizo hapo juu. Wanafanya kazi kwa niaba ya kikundi hicho, sio kwa shirika lao tu, kwa hivyo wanapaswa kuwa na uwezo wa kutoa ushauri bila upendeleo kuhusu vile mambo yanavyofanya kazi. Wafanyakazi wa Ofisi ya Uratibu wa Masuala ya Kibinadamu (Office for the Coordination of Humanitarian Affairs (OCHA)) wanaweza pia kuelezea zaidi kuhusu mfumo wa vikundi nchini mwako.


## Ni miundo mingine gani ambayo ni sehemu ya mfumo wa vikundi?

Katika kila kukabiliana na hali za kibinadamu, vikundi hufanya kazi pamoja katika kundi la uratibu wa vikundi vinavyoongozwa na Ofisi ya Uratibu wa Masuala ya Kibinadamu (OCHA). Wakuu wa Ofisi ya Uratibu wa Masuala ya Kibinadamu (OCHA) na mashirika mengine ya utendaji ya Umoja wa Mataifa, wawakilishi wa mashirika yasiyo ya kiserikali ya ndani, kitaifa na kimataifa, na Harakati ya Msalaba Mwekundu/Red Crescent pia hukutana ndani ya Timu ya Nchi ya Kukabiliana na Hali za Kibinadamu ili kujadili mkakati wa kukabiliana na hali za kibinadamu. Mratibu wa Hali za Kibinadamu anasimamia Timu ya Nchi ya Kukabiliana na Hali za Kibinadamu. Mashirika ya kuongoza vikundi yanawajibika kwa kuibua maswala na changamoto maalum za kikundi pamoja na Timu ya Nchi ya kukabiliana na Hali za Kibinadamu. Wawakilishi wa serikali ya kitaifa na wafadhili pia wanakaa kwenye Timu za Nchi za Kukabiliana na Hali za Kibinadamu.

Timu za Nchi za Kukabiliana na Hali za Kibinadamu na wanachama wao wanaweza kuchukua maswala yaliyowasilishwa na vikundi vya kitaifa kwenda kiwango cha ulimwengu kwa ajili ya kujadiliwa katika Kamati ya Kudumu ya Mashirika Mbalimbali. Kamati hii inaongozwa na Mratibu wa Usaidizi wa Dharura na inawakutanisha wakuu wa mashirika ya utendaji ya Umoja wa Mataifa, Shirika la Kimataifa la Msalaba Mwekundu (the International Federation of Red Cross (IFRC)), Chama cha Kimataifa cha Msalaba Mwekundu (International Committee of the Red Cross (ICRC)) na wawakilishi wa umoja wa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO).

Mbali na vikundi hivyo, pia kuna mipango ya kuratibu hatua na huduma za misaada ya kibinadamu katika sekta nzima. Kwa mfano, wanachama wa Kikundi Kazi cha Mawasiliano na Ushiriki wa Jamii wanaweza kushirikiana kuongeza uwajibikaji kwa na kushiriki kwa watu walioathirika. Nje ya mfumo wa vikundi, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) mara nyingi huratibu, hubadilishana habari na kutetea ndani ya vikao vya kitaifa au vya chini ya kitaifa vya Mabaraza ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO). Mabaraza haya yanaendeshwa na wanachama na kwa pamoja wanakubali masharti yao ya marejeleo na vigezo vya uanachama. Wanaweza kuwa mtandao muhimu wa msaada ikiwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) yanahisi mfumo wa vikundi haushughulikii shida zao. Miungano kadhaa ya Kimataifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO) husaidia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) kujishughulisha na mfumo wa kimataifa wa kukabiliana na hali za kibinadamu. Haya ni pamoja na Baraza la Kimataifa la Mashirika ya Hiari (International Council of Voluntary Agencies (ICVA)), shirika la InterAction, Kamati ya Uendeshaji ya Kukabiliana na ya Hali za Kibinadamu na Mtandao wa NEAR.

Mchoro hapa unaonyesha miundo mikuu ya uratibu ambayo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) yanaweza kushiriki katika viwango tofauti.




## Je, mfumo wa vikundi unatumika kwa migogoro yote katika hali za kibinadamu?

Kwa sababu migogoro ya hali za kibinadamu inatofautiana kwa kiwango na ugumu, uratibu lazima uendane na hali hiyo, na unaweza kubadilika wakati hali ya kukabiliana nazo hubadilika. Mfumo wa vikundi unatumika wakati serikali ya kitaifa ina uwezo mdogo wa kuratibu kukabiliana kwa hali ya kibinadamu na inaalika Umoja wa Mataifa kuongoza huo uratibu. Katika mazingira mengine, mamlaka za kitaifa na serikali za mitaa zinaongoza, wakati mashirika ya Umoja wa Mataifa yanaongoza kwa ushirikiano; katika matukio kama haya, vikundi vya uratibu kawaida huitwa "sekta," sio vikundi. Sekta kwa ujumla hazifaidiki na kiwango sawa cha rasilimali na msaada kama vikundi.

Katika mazingira ya wakimbizi, shirika la wakimbizi wa Umoja wa Mataifa, Kamishna Mkuu wa Wakimbizi wa Umoja wa Mataifa (United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR)), huratibu hatua za kibinadamu, na anaanzisha vikundi vya kisekta ambavyo vinaweza kuongozwa au kuongozwa kwa kushirikiana na mashirika yanayoongoza ya serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) na mashirika mengine ya kibinadamu. Katika muktadha wa uhamiaji uliochanganyika, Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (International Organization for Migration (IOM)), Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhamiaji, linaweza kuchukua jukumu la uratibu. Katika mazingira mchanganyiko, ambapo watu walioathiriwa ni pamoja na wakimbizi, wahamiaji, watu waliokimbia makazi yao (Internally Displaced Persons (IDPs)) na vikundi vingine, vikundi vinaweza kuishi na uratibu wa wakimbizi au uhamiaji. Wakati njia hizi za uratibu zinatofautiana katika utekelezaji wake, kanuni nyingi zilizoonyeshwa katika mwongozo huu zinatumika kwa zote.

## Ni nini kingine ninahitaji kujua?

- Kamati ya Kudumu ya Mashirika Mbalimbali, Moduli ya Marejeleo ya Uratibu wa Vikundi katika Kiwango cha Nchi (2015). Hati hii inatoa ufafanuzi wa kina wa mfumo wa vikundi kama kumbukumbu kwa watendaji wa hali za kibinadamu.
- Kamishna Mkuu wa Wakimbizi wa Umoja wa Mataifa (UNHCR), Mfano wa Uratibu wa Wakimbizi. Ukurasa huu wa wavuti unaelezea mfano wa uratibu wa kukabiliana na hali za wakimbizi wa Kamishna Mkuu wa Wakimbizi wa Umoja wa Mataifa (UNHCR) na jinsi inavyoungana na miundo mipana ya uratibu wa hali za kibinadamu na mfumo wa vikundi.
- Kamishna Mkuu wa Wakimbizi wa Umoja wa Mataifa (UNHCR) - Ofisi ya Uratibu wa Masuala ya Kibinadamu (Office for the Coordination of Humanitarian Affairs (OCHA)), Ujumbe wa Pamoja juu ya Hali Mchanganyiko: uratibu katika mazoezi (2014). Hati hii inaelezea kwa kina mgawanyo wa majukumu kati ya Mwakilishi wa Kamishna Mkuu wa Wakimbizi wa Umoja wa Mataifa (UNHCR) na Mratibu wa Hali za Kibinadamu (Humanitarian Coordinator (HC)) wakati hali tata ya dharura hutokea ambayo inawaathiri wakimbizi.
- Kikundi cha Ulinzi wa Ulimwenguni, Kuunganisha Ulinzi. Ukurasa huu wa wavuti unaelezea jinsi ya kutekeleza kanuni za ulinzi na viungo kwa rasilimali mbalimbali zinazohusiana na ulinzi.
- Baraza la Kimataifa la Mashirika ya Hiari (International Council of Voluntary Agencies (ICVA)), Kanuni za Ushirikiano: Kauli ya Kujitolea. Ukurasa huu wa wavuti una rasilimali nyingi, pamoja na hati kuu ya tafsiri ya Kanuni za Ushirikiano.

Tovuti zingine zenye habari

- Baraza la Kimataifa la Mashirika ya Hiari (ICVA), Masomo ya kutiririsha mtandaoni kuhusu uratibu wa hali za kibinadamu
- Baraza la Kimataifa la Mashirika ya Hiari (ICVA), Masomo ya kutiririsha mtandaoni kuhusu ufadhili wa hali za kibinadamu
- Chuo cha Uongozi wa Kibinadamu, kozi za mtandaoni kuhusu misingi ya kukabiliana na hali za kibinadamu
- Yote katika Kitabu cha Kumbukumbu (All In Diary (AID)), msururu wa muhtasari wa ukurasa mmoja juu ya mambo tofauti ya sekta ya hali za kibinadamu
- Kuunda Nyuma Bora (Building Back Better), kozi ya mtandaoni kuhusu hali za muingiliano na ikiwa ni pamoja na utangulizi wa kanuni na viwango vya Nyanja (Sphere)
- DisasterReady.org, rasilimali zaidi ya 600 za mafunzo zinazoangazia mada kuu kwa sekta ya hali za kibinadamu
- Fedha za Watoto za Umoja wa Mataifa (United Nations Children's Fund (UNICEF)), Mafunzo makuu kuhusu uratibu ya Kikundi cha Elimu Duniani

Kwa maelezo zaidi yanayohusiana na uratibu wa Kikundi cha Elimu, unakaribishwa kuwasiliana na Kikundi cha Elimu Duniani Ofisi ya Usaidizi au tuma barua pepe kwa Kemal Alp Taylan, Mtaalamu wa Ujanibishaji, kemal.alptaylan@savethechildren.org.

## Vifupisho muhimu vya uratibu

Hifadhidata ya nani anafanya nini wapi na lini
- (3W / 4W - Database of who does what where and when)
- AAP - Uwajibikaji kwa Idadi ya Watu Walioathirika
- AoR - Eneo la Wajibu
- CAP - Mchakato wa Rufaa Zilizojumuishwa
- CBPF - Mfuko wa Fedha za Pamoja za Nchi
- CCRM - Moduli ya Marejeleo ya Uratibu wa Vikundi
- CERF - Mfuko Mkuu wa Fedha za Kukabiliana na Hali za Dharura
- CLA - Shirika Linaloongoza Vikundi
- ERC - Mratibu wa Usaidizi wa Dharura, mkuu wa Ofisi ya Uratibu wa Masuala ya Kibinadamu Duniani (OCHA)
- ERP - Utayari wa Kukabiliana na Hali za Dharura
- GCCU - Kitengo cha Uratibu wa Vikundi Duniani
- GCLA - Shirika Linaloongoza Vikundi Duniani
- GEC - Kikundi cha Elimu Duniani
- GHP - Jukwaa la Hali za Kibinadamu Duniani
- GPC - Kikundi cha Ulinzi Duniani
- HC - Mratibu wa Hali za Kibinadamu
- HCT - Timu ya Nchi ya Hali za Kibinadamu
- HNO - Muhtasari wa Mahitaji ya Kibinadamu
- HPC - Mzunguko wa Programu ya Hali za Kibinadamu
- HRP - Mpango wa Kukabiliana na Hali za Kibinadamu
- IASC - Kamati ya Kudumu ya Mashirika Mbalimbali
- ICVA - Baraza la Kimataifa la Mashirika ya Hiari
- ICCG / ISCG - Kikundi cha Uratibu wa Vikundi Mbalimbali au Sekta Mbalimbali
- IM - Usimamizi wa Maelezo
- IMO - Afisa wa Usimamizi wa Maelezo
- INEE - Mtandao wa Mashirika Mbalimbali kwa Mafunzo ya Hali Dharura
- INGO - Shirika Lisilo la Kiserikali (NGO) la Kimataifa
- MIRA - Tathmini ya Awali ya Haraka ya Sekta Mbalimbali
- MSNA - Tathmini ya Mahitaji ya Sekta Mbalimbali
- NDMA - Shirika la Kitaifa la Kukabiliana na Maafa
- NGO - Shirika Lisilo la Kiserikali
- OCHA - Ofisi ya Uratibu wa Masuala ya Kibinadamu
- POLR - Mtoaji wa Hatua ya Mwisho
- SAG - Kikundi cha Ushauri wa Kimkakati
- SCHR - Kamati ya Uendeshaji katika Kukabiliana na Hali za Kibinadamu
- Sitrep - Ripoti ya Hali
- SOP - Utaratibu wa Kawaida wa Uendeshaji
- TEG - Kikundi cha Wataalam wa Mada
- ToR - Masharti ya Marejeleo
- TWG / TWiG - Kikundi cha Kazi ya Ufundi
- UNHCR - Kamishna Mkuu wa Wakimbizi wa Umoja wa Mataifa
- UNICEF - Fedha za Watoto za Umoja wa Mataifa